# *TUMTENDEJE HUYU YESU AITWAYE KRISTO?*

. . .alasiri, nataka kuharakisha, kwa sababu ninajua kwamba ninyi nyote mmechoka kutokana na kuwepo kanisani, (asante, bwana), kuwepo kanisani leo. Nataka tu kuchukua wakati huu mdogo, hata hivyo, kuonyesha shukurani zangu kwa ndugu Demos Shakarian.

2 [Sehemu tupu kwenye ukanda—Mh.] . . .hatujawahi kukutana kama Pentekoste, katika vikundi. Kuna tofauti nyingi mno. Bali kuna mahali pamoja ambapo tunashiriki pamoja, chini ya Damu ya Yesu Kristo, hapo ndipo ambapo tunashiriki pamoja. Hiyo ndiyo njia ya Mungu kwa sisi kukutana, kwa vyo vyote. Na hakuna mahali pengine ambapo Mungu aliahidi kukutana na mwanadamu, ni chini tu ya Damu iliyomwagika.

3 Nilikuwa ninafikiria usiku uliopita kumhusu ndugu yetu, Oral Roberts, alipotamka maneno yale mazuri sana hapa, kuhusu, "Toka utu wake wa ndani kabisa itatoka mito ya maji." Ile kuu. . .Jinsi yeye alivyoliingiza hilo, kuhusu, "ndani yake," ninaamini yeye alisema, "itatoa, itatoka mito hii ya maji."

4 Umewahi kuchunguza, ni mito ya maji aina moja? "Mito," wingi; "maji," aina moja. Si mito ya maji aina mbalimbali; bali "mito ya maji," Roho mmoja, "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Mwili ule ule." Ndani Yake hububujika wema na neema ya Mungu.

5 Na sasa, ninyi watu wa California, tutakuwemo katika mkoa wenu, kuanzia juma lijalo, nadhani, huko. Na hata kuendelea kupitia Georgia, Louisiana, Florida, na kuendelea mpaka tuanze kuzuru nchi za ng'ambo.

6 Bwana awabariki, mno. Ninafurahiwa na bibi wadogo ambao wamecheza muziki ule, na watu hawa wazuri niliokutana nao.

7 Huyu ndugu mgeni hapa, Ndugu Solomon King. Naweza niseme hilo vibaya. Naweza kumwazia Mfalme Sulemani na kuligeuza tu. Hilo lilikuwa wakati huo, huyu ni mfalme mwingine, pia. Hilo ni kweli. Mwana wa Mfalme, kwa vyo vyote, hilo ni kweli; mwana wa Mfalme fulani; wala sio mfalme *fulani, yule* Mfalme!

8 Niangaliapo hili, linanikumbusha habari za huku Mexico, miaka michache iliyopita huko Mexico City. Tulikuweko huko usiku mmoja, kulikuwa na mwanamume kipofu, usiku uliotangulia, aliyekuja jukwaani, kipofu kabisa kabisa kwa

miaka mingi. Nikaangalia miguu yake. Nilikuwa nimesimama pale nimevalia suti nzuri, jozi ya viatu, nami nikaangalia yake. Yeye alikuwa kipofu, hana viatu, suruali iliyochakaa, naye amesimama nje huko kwenye mvua. Lo, pengine elfu thelathini, au zaidi, nao wamesimama nje huko kwenye mvua, wakiegemeana, hamna viti; wamekuwepo hapo tangu mapambazuko wakingojea tu kuingia humo usiku ule. Na palikuwepo na huvu mwanamume kipofu, aliyepata kuona.

9 Na usiku uliofuatia, vingi, kama mara mbili ya ukubwa wa benchi hili hapa, cho chote tungekiita, vilikuwa tu kwenye jukwaa, vilikuwa tu lundo la urefu karibu pale panaponing'inia pazia lile, la shali kuu kuu na makoti, na ambayo watu wameyavaa na wameyatupia juu hapo. "Ili tu tuviguse!"

Karibu wote walikuwa Wakatoliki, bila shaka, kule Mexico City.

10 Nami niliingia, nikiwa Mprotestanti wa kwanza aliyewahi kuja chini ya mwaliko wa kijeshi. Hilo lilikuwa toka kwa Jenerali Valdivia, rafiki yetu mzuri hapa, Wafanyi Biashara wa Injili Yote.

11 Nakumbuka usiku ule, kulitokea kiyowe huko nje. Na mwanangu akanijia, akasema, "Ninao bawabu karibu mia moja na hamsini, au zaidi, wamesimama huko, na hawamwezi mwanamke mdogo wa Kihispaniola. Ana mtoto aliyekufa, alikufa asubuhi hii." Kasema, "Hawawezi kumzuia mwanamke yule." Kasema, "Atapanda juu ya migongo yao na kila kitu."

Nami nikasema, "Vema, iimarishe tu."

Akasema, "Sina kitu cho chote kingine cha kuiimarishia nacho."

Nikasema, "Mpe kadi ya maombi."

Akasema, "Sina kadi. Zote zimetolewa."

12 Nikasema, "Ndugu Moore, nenda ukamwombee," nikasema, "maana yeye hanijui mimi." Nikasema, "Nenda wewe ukamwombee. Nami nitajaribu kuombea hili lundo la nguo, hivi punde tu."

13 Na wakati nilipokuwa nimesimama pale, nilitazama juu ya makutono *hivi*, na mbele yangu alikuwepo mtoto mchanga wa Kimexico, hana meno, akitabasamu tu, moja kwa moja mbele yangu. Nikasema, "Ngojea kidogo, Ndugu Moore."

14 Nao wakamleta yule mtoto. Na yule bibi mdogo akaingia, akianguka chini, na mkononi mwake ana msalaba. Nikasema, kupitia kwa ndugu, mkalimani, amwambie asimame.

15 Nami nikasema, "Ndugu Moore, sijui kama hili ndilo jambo lenyewe, au la, bali niliona kitoto kichanga kimesimama mbele yangu, katika ono sasa hivi, kinatabasamu."

16 Alikuwa amemfunika kwa blanketi dogo, ya samawati na jeupe, yenye milia, amelowa tu maji. Ilikuwa inanyesha tu. Ilikuwa mnamo saa nne usiku. Mtoto yule alifariki asubuhi ile, kwenye saa mbili au tatu, katika ofisi ya daktari, kwa niumonia. Na kwa hiyo yeye alikuwa amesimama kwenye mvua. Nywele zake zilikuwa zote zimeshuka usoni mwake, na, na yeye alikuwa mtoto wa kike mzuri sana. Alionekana kuwa labda, mtoto wake wa kwanza, ilionekana kama yeye ana miaka ishirinina kitu. Na yule mtoto alikuwa amekufa.

17 Nami niliweka tu mikono yangu juu yake, na nikasema, "Bwana Yesu, Mimi sifahamu jambo hili, bali kulingana na ono lile nililoona . . . " Na niliposema hilo tu, alipiga mateke na akapiga kiyowe, na yule mtoto akawa mzima.

18 Na nilikuwa na Ndugu Espinoza. Wangapi wanamjua Espinoza, Ndugu Espinoza? Ndiye aliyefuatilia jambo hilo, kwenye afisi ya daktari, akaona kwamba ni kweli, unaona, hilo ni kweli, mtoto yule alikufa asubuhi ile, kuwekea sahihi kile cheti.

19 Na kwa hiyo sasa Yeye ni Mungu yeye yule leo, kama tu tungekuwa na aina ile ile ya imani katika Yeye. Hilo ni kweli.

20 Baba yetu wa Mbinguni, tupelekee imani ile ya yule mwanamke wa Kimexico, leo. Yeye alimwona yule mwanamume mdogo kipofu ameponywa, usiku uliotangulia. Akisimama nje kule akiwa na mtoto wake mchanga, katika upepo ule baridi, uliovuma, alishikwa na niumonia. Na asubuhi iliyofuatia, mapema, alikufa katika afisi ya daktari. Wazo lake la kwanza likaja, "Kama Mungu anaweza kuponya macho yaliyopofushwa, anaweza kufunua mawazo ya moyo, bado lingali Neno la Mungu, kwa maana Neno la Mungu huyatambua mawazo yaliyoko moyoni." Na yeye alijua kwamba Yeye aliweza kutambua mawazo ambayo yalikuwa moyoni mwake. Alimwamini Yeye, na ya kwamba Yeye aliweza kumfufua Lazaro kutoka kaburini, na Yeye alikuwa yeye yule jana, leo, na hata milele. Alikuja na Wewe ulimtunukia, Bwana, kwa kumrudishia mtoto wake mchanga. Anaishi leo, kadiri tujuavyo. Tunakushukuru Wewe kwa jambo hili.

21 Tubariki, leo, Baba. Bariki watu hawa walio na vitambaa hivi na makoti yaliyopo hapa, pia. Na jalia Roho Wako Mtakatifu aje sasa na atufunulie Neno la Mungu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

22 Najua mna mkutano katika muda mfupi tu, au saa kumi na moja, naamini. Na kwa kawaida hilo halingenipa wakati wa kuanza, lakini nime—nimeongoka katika jambo hilo, nafikiri, sasa. Nimejitahidi sana juma hili, nikiwa na homa, labda hilo lilikuwa linatenda kazi kwa manufaa.

23 Niliwaambia watu majuzi yale, ni—nilijipatia kibandiko cha nywele, lakini niliona aibu kukivaa kwa sababu niliwapigia

makelele wanawake sana kuhusu nywele zao. Na nywe—nywele zangu ziling'olewa na asidi ya kaboni. Na majuzi usiku walifungua mlango ule, hewa kidogo iliingia kupitia hapa, nami sikudhania ningerudi leo. Nilisema, "Kama Oral Roberts yuko hapa, anaweza kujitayarisha, akiweza." Hajatokeza bado, kwa hiyo nitasoma Maandiko, nanyi mniombee.

24 Mathayo Mtakatifu, sura ya 27, kuanzia na aya ya 11, napenda kusona. Sasa sikilizeni kwa makini sana somo la Neno. Sababu, neno langu ni neno la binadamu, litashindwa. Neno Lake haliwezi kushindwa, kwa hiyo sasa sikilizeni kwa makini tunaposoma.

25 Na kabla, wakati mnapofungua, ningetaka kutangaza kwamba ndugu yetu, Oral Roberts, atakuweko Yerusalemu, pia, usiku wa Ijumaa ijayo, kwa hiyo nyote mnaotaka kuja. Unasema "Wapi?" Mtu fulani alisema Florida ilikuwa nchi ya ahadi, nadhani naweza kuita Tucson, Yerusalemu. Phoenix iko bondeni, unaona, na Yeriko iko chini tu bondeni toka Yerusalemu. Sitatoka kamwe hapa jinsi hiyo, sivyo? Ndugu Oral Roberts anazungumza usiku wa Ijumaa ijayo na nina hakika ninyi nyote mtafurahia kumsikia. Tutafurahi mkija kule.

26 Sura ya 27, aya ya 11.

> *Naye Yesu akasimama mbele ya liwali; liwali akamwuliza, akasema, Wewe ndiwe Kristo wa Wayahudi? Yesu akamwambia, Wewe wasema.*
>
> *Lakini aliposhitakiwa* (kwa wakuu) *na makuhani na wazee,* na wale. . .na *hakujibu hata neno.*
>
> *Ndipo Pilato akamwambia, Husikii ni mambo mangapi wanayokushuhudia?*
>
> *Asimjibu hata neno moja, hata liwali akastaajabu. . .*
>
> *Basi wakati wa siku kuu, liwali*. . .kwa. . . *huwafungulia mkutano mfungwa mmoja waliyemtaka.*
>
> *Basi palikuwa na mfungwa mashuhuri siku zile, aitwaye Baraba.*
>
> *Basi walipokutanika, Pilato akawaambia, Mnataka niwafungulie yupi? Yule Baraba, au Yesu aitwaye Kristo?*
>
> *Kwa maana alijua ya kuwa wamemtoa kwa husuda.*
>
> *Na alipokuwa ameketi juu ya hiki, ameketi juu ya kiti cha hukumu, mkewe alimpelekea mjumbe, kumwambia, Usiwe na neno na yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake.*
>
> *Nao wakuu wa makuhani na wazee wakawashawishi makutano ili wamtake Baraba, na kumwangamiza Yesu.*

*Basi liwali akajibu, akawaambia, Mnataka niwafungulie yupi katika hawa wawili? Wakasema, Baraba.*

*Pilato akawaambia, Basi, nimtendeje Yesu aitwaye Kristo? Wakasema wote, Asulubiwe.*

*Akasema,* liwali,*. . . ni ubaya gani alioutenda? Wakazidi sana kupiga kelele, wakisema, Na asulubiwe.*

*. . . Pilate alipoona ya kuwa hafai lo lote, bali ghasia inazidi tu, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya mkutano, akasema, Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki: yaangalieni haya ninyi wenyewe.*

*Watu wote wakajibu wakasema, Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu.*

*Ndipo akawafungulia Baraba; na baada ya kumpiga Yesu mijeledi, akamtoa ili asulubiwe.*

27 Somo langu leo, kama ningeliita hivyo, kwa dakika thelathini zinazofuata, ni: *Tumtendeje Huyu Yesu Aitwaye Kristo*? Na basi ningependa kusema hili, pia. "Yesu mikononi mwetu."

28 Sasa, ninaamini kwamba saa ile ambapo tukio letu linaanza, ni mnamo mchana, katika mahakama ya Pilato. Nao ni mmoja wa nyakati za huzuni sana, na mmoja wa nyakati ngumu sana, za historia yote. Lilikuwa kosa la kusikitisha sana ambalo kanisa liliwahi kufanya katika historia yake. Walikuwa wameishalitenda, na sasa limekwisha tupwa pajani mwa liwali, serikali. Vyote viwili kanisa na serikali, kwa sababu walikuwa watu waliochaguliwa na Mungu, walioitwa kuwa watumishi Wake, nalo taifa lilipaswa litawaliwe na amri za Mungu.

29 Nalo kanisa lilikwisha mkataa Masihi wao. Ingawa Yeye alikwisha dhihirishwa vizuri sana kwao, wao wamechagua afadhali wadumua katika desturi za wazee za siku ile, kuliko kuliamini Neno lililotiwa mafuta na kuthibitishwa, ambalo Mungu aliwaahidi kwa mamia ya miaka, litakuja.

30 Mmechunguza, pia ilitabiriwa kwamba wangepofushwa? Hawakuweza kuelewa jambo hili, na ambavyo wangepofushwa, lakini walikuwa wamepofushwa.

31 Nao walifanya kosa lao kubwa, na siku hii walilionyesha kwa mara yao ya mwisho. Na sasa limo mikononi mwa serikali, na sasa serikali yapaswa ijichagulie. Makanisa yalikuwa tayari yamemkataa Yeye, ingawa Mungu tayari amethibitisha kwelikweli kwamba Yeye alikuwa Masihi wao.

32 Sasa nataka kuchukua muda mchache kabla ya kuliingilia hili, kwenye kifungu na kadhalika, hata nina maelezo niliyoandika hapa kuhusu jambo hilo. Vipi watu wale walishindwa kuliona hilo? Jambo moja Maandiko yananena

waziwazi, "Walikuwa vipofu." Lakini ni vigumu kuwafanya waelewe walikuwa vipofu, kama tu ilivyo vigumu leo.

33 Ambapo, Biblia hutuambia kwamba kizazi hiki ni "uchi, chenye mashaka, masikini, na kipofu, na hakijui hilo." Sasa, hayo ni Maandiko. Sasa unatuambia sisi Waamerika tu vipofu, tutakuambia mara moja wewe hujui unachokizungumzia.

34 Bali mimi nitawapelekeni mahakamani alasiri ya leo, muone kama tu vipofu au la. Nasi tunamhukumu Yesu, alasiri ya leo, na Damu Yake mikononi mwetu, na sasa tunataka kuona tutatenda nini kuhusu jambo hilo. Je tutafanya kosa lile lile la kijinga walilotenda wakati huo?

35 Angalia kilichotukia. Alikwisha thibitishwa waziwazi, naye alitimiza kazi ambayo Mungu alisema Yeye angetimiza, kama Masihi. Hakukuwa na swali kuhusu jambo hilo. Maana, Yeye alizaliwa jinsi Mungu alisema angezaliwa. Akakataliwa jinsi Mungu alivyosema Yeye angekataliwa. Alithibitisha kuwa Yeye ni Masihi, kwa sababu Masihi alikuwa Mungu. *Masihi* humaanisha "aliyetiwa mafuta." Na Yeye alipakwa mafuta na ule—na utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake. Yeye hakuwa tu nabii. Hata hivyo, Yeye alikuwa Nabii, bali Yeye alikuwa zaidi ya nabii. Alikuwa Uungu ukikaa katika mwanadamu kwa jinsi ya mwili, akijulikana kama Mwana wa Mungu. Mungu, Baba, alimfunika kama kivuli bikira na akaumba ndani yake, Damu, katika tumbo lake la uzazi, chembe ya Damu ambayo ilimzaa Mwana wa Mungu, ambamo Mungu alifanya maskani.

36 Naye alikuwa amethibitishwa kwao, jinsi Yeye alisema alikuwa, bali Yeye kamwe hakutoka akaja moja kwa moja na kuwaambia, "Mimi ni Mwana wa Mungu." La, la. Yawabidi kuamini hilo. Yeye alisema, "Kazi zangu hushuhudia Mimi ni Nani." Yeye akawaamuru, "Angalieni katika Maandiko," waone ni siku gani walikuwa wanaishi, basi wangejua Yeye alikuwa nani.

37 Nafikiri ingetupasa kutenda jambo hili, tunapoona kutoka kwingine kumewadia. Nadhani tungeangalia, na kuyachunguza Maandiko, tunapoona mambo haya yakitokea.

38 Tunaona basi kwamba kanisa limefanya uamuzi wao, kwamba hawakutaka kujihusisha kwa cho chote Naye. Mbona, ambapo Neno kwa usahihi lilimtambulisha Yeye, na kazi Zake zilithibitisha kwamba Yeye alikuwa Masihi? Jambo la kutisha namna hiyo, jambo muhimu, kosa, ambalo kanisa lile lilitenda!

39 Nami nashangaa kama ingewezekana kwamba tungeweza kufanya kosa lile lile? Walikuwa wamekwisha pewa nafasi yao ya mwisho kuona Yeye alikuwa nani, na kulikubali Hilo. Sasa, si sikuzote hutakuwa na nafasi ya kukubali anachotuma Mungu. Unaona, subira Yake hatimaye huisha, halafu unavuka ule

mstari baina ya neema na hukumu. Hakuna kitu kinachosalia ila hukumu wakati subira ya Mungu hatimaye inakwisha.

40 Lakini wao walikwishapewa nafasi hii, nao wamekwishamwona Yeye akijitambulisha Mwenyewe, wakamwona Yeye penye kile kisima pamoja na yule mwanamke, na akamwambia yeye kwamba alikuwa na wanaume watano. Alimwona Nathanaeli akija Kwake, baada ya Filipo kwenda na kumleta Nathanaeli kwenye Uwepo Wake, na Yeye akanena na kusema sawasawa kabisa yeye alikuwa ni nani na ametoka wapi. Akamwambia Simoni Petro baba yake alikuwa ni nani, na jina lake ni nani. Na hawakuwa na nabii kwa mamia ya miaka.

41 Na hata yule mwanamke mdogo kahaba alitambua Neno la Mungu. Yeye hakuwa amechanganyika kabisa katika kitu fulani. Yeye, yeye, vema, akili yake haikuwa kabisa, ambacho tungeweza kuita, kama mngenisamehe kwa kutumia maneno haya, "aliyechanganyikiwa," akikimbilia *hapa* na kukimbilia *pale*. Bongo lilikuwa bikira, kadiri hilo linavyohusika. Akasema, "Tunajua kwamba yuaja Masihi, na hili ndilo ambalo Yeye atatenda."

Na Yeye akasema, "Mimi Ndiye."

42 Na haraka akakimbia, akawaambia watu wa mjini, "Njoni, mumtazame Yeye, huyu ndiye Masihi hasa."

43 Mbona, wale waalimu na watu wa zamani zile hawakuweza kuona hilo. Hilo ni, ingekuwa vigumu kuona kama usingejua Maandiko. Lakini Maandiko yalisema, "Walikuwa wamepofushwa." Kwa kweli walipofushwa. Lakini walichagua, afadhali, badala ya yule Yesu aliye mwema sana, kwenye... Tunasikia kelele zikitoka, "Msulibishe!"

44 Pilato alisema, "Nimtendeje huyu Yesu aitwaye Kristo?"

Wakasema, "Mwondolee mbali! Msulubishe!"

"Niwafungulie yupi, Baraba au Yesu?"

45 Nao wakafanya kosa la kijinga kwa kumchagua muuaji badala ya Mtoa-Uzima. Mmoja ambaye ametambulika kama Mtoa-Uzima, walimchagua muuaji ambaye alitambulikana kama muondoa-uzima. Tofauti jinsi gani! Nami nashangaa kama...

46 Ninalinena hili kwa uchaji wote wa kiungu kwa ndugu zangu na dada zangu, na kwa wanaume na wanawake wa siku hii, ambao ninawahubiri, nikiwa na upendo moyoni mwangu kwa watu wote: ninashangaa kama hatuko karibu tayari kuona jambo lile lile kama waliloona wakati huo! Serikali ilihusika katika jambo hili, na swa—swala lilikuwa linaendelea. Swali lazima litatuliwe. Lilifikia kwenye uamuzi wa mwisho.

47 Ndivyo imekuwa leo, ndivyo ilivyo katika saa hii! Shindano la mwisho linaendelea. Lazima jambo fulani lifanywe, yakubidi

useme “ndiyo” au “la.” Lakini, kumbuka, haitakuwa wakati unapolazimishwa kulitenda. Yakubidi kulitenda kwa hiari yako sasa. Sasa! Siyo wakati huo unapowadia; utakapowadia, imekwisha. Sasa! Hii inaweza kuwa siku ya mwisho utakuwa na wakati wa kujiamulia. Huwezi kulitenda wakati huo, umekwisha ichukua tayari, ni mbali mno, wakati huo. Yakubidi ulitende sasa. Usingojee hadi dakika ya mwisho, kwa sababu mashua itang’oa nanga na kukuacha, na milango itafungwa.

48 Watu wengi wangaliingia katika safina kama wangalifika pale, mvua ilipoanza kunyesha. Bali uamuzi ulikuwa umefanywa, Injili imehubiriwa, ishara zikaonyeshwa; na wakati umekwisha, mvua ilikuwa inanyesha wakati huo, hukumu imeanza.

49 Naam, taifa zima lililazimika kumkataa Yeye, kwa sababu kwamba liliitwa, kama tungesema leo, “taifa la Kikristo,” kama hili liitwavyo taifa la Kikristo. Kwa hiyo, kama liliitwa taifa la Yehova, watu Wake waliochaguliwa, halafu ilibidi taifa zima limkatae. Kanisa lilikwisha kumkataa Yeye. Kanisa lilikwishamtupa Yeye nje. Hawakutaka kujihusisha na Yeye, lakini sasa serikali inahusika katika hilo.

50 Hivyo limerudi tena, limerudi moja kwa moja pajani tena, Maandiko yakiwepo hapa, yamethibitishwa, sawasawa tu kabisa na ambalo Yesu alisema lingetukia. Kwa nini tunasitasita katika saa hizi za giza? Kwa nini tuachilie hili lije juu yetu, wakati tumeonywa kwelikweli? Kama tu ilivyokuwa katika siku za Lutu, tunaona jambo lile lile. Yehova ameonyesha vile ilivyo, na kutuambia, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu!” Mnawaona wajumbe nje huko Babeli, wakijaribu kumtoa Lutu nje, na mnaona Ujumbe kwa Mteule, Ibrahimu, ambaye alikuwa tayari ametoka. Na kila kitu, sawasawa kabisa, hata na jina, mahali, na wakati, vimethibitishwa kwelikweli.

51 Lakini sasa limo katika mikono ya serikali. Serikali yabidi ilihukumu sasa, na watafanya hivyo. Usifadhaikie jambo hilo. Ni taifa la Kikristo, inalibidi lichukue msimamo wake wa Kikristo kama ndivyo lilivyo. Uamuzi wa mwisho unaendelea.

52 Ilibidi taifa zima lifikishwe hukumuni. Kwa sababu, ilitukia mnamo AD 70, wakati yule jenarali maarufu wa Kirumi, Titus, alipouzingira Yerusalemu, mnamo AD 70, akiwa na jeshi lake kutoka Rumi, na hapo walilipa gharama ya kumkataa Yeye.

53 Leo, tunapoangalia hukumu ile pale, nasi tunatoka hapa na kuiigiza katika njia mbalimbali, za hukumu Ijumaa Kuu, na kulizungumza, na kadhalika. Na jambo lile lile ambalo tunalizungumzia, ambalo lilitukia Ijumaa Kuu, lipo mbele zetu kabisa leo! Na wazee wetu wanatenda jambo lile lile hao walilotenda, wakilichukua katika hukumu ya namna ile ile, baada ya Neno la namna ile ile lililoahidiwa la siku hii kwisha kuthibitishwa namna ile ile tu kama lilivyothibitishwa kule.

54 Yesu, "mvulana wa kawaida wa seremala," kama ilivyofikiriwa. Yeye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa. Na Yeye alitambulishwa kikamilifu, kwa sababu kazi za Mungu zilidhihirishwa zenyewe kupitia Kwake, na kuthibitishwa kwamba Yeye alikuwa Masihi.

55 Na, leo, kesi ya aina ile ile imerudi tena, ambapo Roho Mtakatifu amekuja juu yetu katika siku za mwisho na kujitambulisha Mwenyewe katikati ya kanisa letu, na amehakikisha kazi zile zile ambazo Yeye amefanya Yeye alipokuwepo hapa katika utimilifu juu ya Yesu Kriso. Yeye ametenda jambo lile lile juu ya Bibi Arusi, akifanya jambo lile lile, na bado tunataka tuliondoshe Hilo.

56 Kumbuka, hizi ni kanda ambazo zinatengenezwa sasa, ambazo zinaenda ulimwenguni kote, sio tu Phoenix hapa. Ninazungumzia nusu ya ulimwengu, wakati huu, sababu tuna huduma ya kanda inayozunguka ulimwengu.

57 Angalieni, leo tuna hukumu ya aina ile ile, baada ya Neno lile lile lililotambulishwa. Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Mtakatifu Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Mathayo 28, "Ulimwenguni kote, hubirini Injili kwa kila kiumbe." "Tazama, bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena; bali ninyi mtaniona Mimi, kwani nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa wakati." "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele!"

58 Wamechagua leo, sio tu muuaji, bali muuaji wa Neno, kibaraka wa yule muuaji wa kwanza kabisa.

59 Wakati wao, mitume walikuwa wanahubiri Injili, na kuja kupitia kwa Ireneo, na wengi wa wakufunzi maarufu na waanzilishi wa kule nyuma katika wakati wa mwanzoni, ilifikia kule Nikea, wakati mmoja, kwa uamuzi wa mwisho, nao wakaamua kufanya kanisa la ulimwengu mzima, kuwashurutisha watu kuja chini ya mamlaka yao. Wengi ambao wamesoma historia hapo, wanajua manabii wengi wa zamani walikuja pale wamevaa ngozi, wakila mboga tu na kadhalika, nao walijaribu kushikilia Neno lile, kushikilia Neno la Mungu. Lakini walifanya nini siku zile kumi na tano za siasa za kikatili? Hatimaye waliamua kuunda kanisa la ulimwengu mzima, na kupandikiza baadhi ya upagani na Ukristo, na kulipeleka kama kanisa la ulimwengu mzima.

60 Na, leo, Waprotestanti wanajikusanya pamoja katika Halmashauri ya Ekumeni, wakifanya jambo lile lile, wakipandikiza desturi ya binadamu, na badala ya kuchukua Neno la Mungu ambalo limethitishwa kikamilifu na Roho Mtakatifu, kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kanisa linasimama katika mizani, leo, na linaonekana limepungukiwa. Mmerudi kwenye mahakama ya Pilato. Ndiyo, bwana.

61 Linafanya nini? Linafanya sanamu ya mnyama. Ni kibaraka wa Rumi. Wakati Halmashauri ya Ekumeni inashurutisha, na itashurutisha kila madhehebu ya Kiprotestanti yajiunge nalo; na kwa kweli yote yamo mle sasa, Full Gospel na yale yote. Na saa itafika wakati itawalazimu kuja au kukaa nje, na, wakati huo, shurutisho hilo lijapo, tayari umekwisha jitambulisha na alama ya mnyama. Naam, hilo ni kweli kabisa.

62 Ni nini? Makahaba wa Kiprotestanti na yule mama wa kale, Rumi, kahaba! Ufunuo 17 imesema alikuwa hivyo, "MAMA WA MAKAHABA," barabara, madhehebu ya Kiprotestanti; akishikilia mkononi mwake kikombe cha ghadhabu ya—ya Mungu, cha kutakia heri, ushuhuda wake, "*hili* ndilo tunaloamini," na kila mmoja, "*hili* ndilo tunaloamini."

63 *Hili* ndilo kanisa lapaswa kuamini, Neno la Mungu, "na kila neno la mtu liwe uongo." Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa.

64 Lakini tunamleta Kristo tena kwenye saa ile kuu muhimu ambapo Yeye alisimama, katika ukumbi wa hukumu wa Pilato, kwa kusikitisha, kundi dogo limesukumiwa kando, na kichwa kimeinamishwa. Madhehebu mengine yamewakana, yamewakataa, na kuwafukuza, na kusema, "Msijihusishe na jambo Hilo!" Afadhali ulichunguze na Neno. Sasa tunaona, hii Halmashauri ya Ekumeni ilivyo. Inafanya nini? Hilo, Biblia . . .

Unasema, "Biblia inanena kuhusu jambo hilo?" Ndiyo.

65 "Wakiwa na mfano wa utauwa bali wakikana Nguvu zake." Vipofu, uchi, waendao kanisani, wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu za Roho Mtakatifu ambaye humtambulisha Yesu Kristo kwenye Neno Lake. Mtu anawezaje kudai kuwa ana Roho Mtakatifu na kukana Neno hasa ambalo ni Roho Mtakatifu? Mtu anawezaje kutenda jambo hilo? Ushuhuda wake mwenyewe unashuhudia kwamba yeye hayuko kama anavyopaswa kuwa, akifanya uzinzi wa kiroho, akikana Nguvu za Mungu. Paulo alisema, katika Timotheo wa Pili, sura ya 3, hivyo ndivyo itakavyokuwa, kasema, "Watakuwa wakaidi, wenye kujivuna!"

66 "Nina shahada ya daktari, Ph.D., L.L.D." Kwangu mimi, hivyo ni kuwa mbali zaidi na Mungu kuliko ulivyokuwa wakati ulipoanza. Ndiyo, bwana. Hizo zinakutoa tu kwa Mungu, hazikuleti kwa Mungu. Kitu kimoja tu kinaweza kukuvuta kwa Mungu, na huyo ni Roho Mtakatifu, kwa Neno Lake.

67 Roho Mtakatifu ni dira. Nyota ya Kaskazini ni Neno. Na dira itaelekeza tu kwenye Nyota ya Kaskazini. Na Roho Mtakatifu atakuelekeza tu kwenye Neno, si kwenye mwenendo wa ekumeni fulani, si madhehebu fulani, bali kwenye Neno la Mungu. Kumbuka, nyota zote husogea pamoja na dunia, lakini Nyota ya Kaskazini hukaa papo hapo, kwa sababu iko katikati. Na kila neno la mtu mwingine litashindwa, bali Neno la Mungu haliwezi kushindwa. Ni Nyota ya Kaskazini, imewekwa katikati. Hiyo

haitasogea pamoja na dunia. Haidhuru dunia iko wapi. Hiyo hudumu ile ile jana, leo, na hata milele. Na Yeye ni Neno!

68 Ndugu na dada, ninawasihi, katika Jina la Yesu, kufikiria jambo hili. Mumeniamini mimi katika yale niliyosema katika miaka hii. Kama Mungu amethibitisha kwamba yale niliyosema yamekuwa Ukweli, si mimi, ni Neno Lake ambalo limetenda jambo hilo, basi ninawasihi, katika Jina la Yesu, kuchunguza jambo Hili. Msiwe vipofu kwa mambo haya; yako juu yenu.

69 Na, kumbukeni, Biblia ilisema katika Mathayo 24:24! Kwamba, "Wote ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana Kondoo, tangu kuwekwa misingi ya dunia, wangechukua alama hii." Mteule tu, ambaye amechaguliwa kuona jambo Hilo, ataliona. Wengine wote watalikosa maili milioni moja.

70 Twaona ushawishi mkubwa umeandaliwa sasa, mtambo mkubwa wa Shetani umewekwa tayari. Kitu unachohitaji ni. . . Una mitambo, unangojea tu nguvu za kuuendesha uanze kutenda kazi. Ushawishi huo ni kusanyiko lote, halmashauri kubwa na kadhalika. Mtambo ule mkubwa umekaa pale, bali wanangojea ile saa ambayo kizibo kitakapoondolewa, ndipo wanaweza kulitekeleza, na kulilazimisha, kulifanya sheria. Tazama matangazo na mambo tunayoyasikia leo, kwenye redio na magazetini. Mbona, lipo karibu nanyi sasa hivi.

71 Hatuna muda wa kutenda kitu kingine ila kumpokea Yesu Kristo, Yeye amekwisha tambulishwa kinaganaga.

72 Sikiliza, tunazungumza kuhusu mtambo mkubwa wa Shetani juu kule, tayari kuanza kazi, hilo ni kweli, kupondaponda; bali, kumbuka, kundi dogo la Mungu ambalo linaamini Neno, mitambo yake iko tayari pia. Iko tayari kwa nguvu za kuliwasha moto kwa Roho Mtakatifu. "Msiogope, kundi dogo, ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa ule Ufalme." Roho Mtakatifu atawasha Kanisa dogo ambalo limetoka ulimwenguni, wanawake wenye nywele ndefu, Mnadhiri, kuthibitisha wamejitenga na . . .

73 Mnadhiri ni (mtu ambaye nini?) mtu anayejitenga, kwa ajili ya Neno la Mungu; sio wavaao kaptura, akina Yezebeli waliopoda nyuso zao, huku wanajiita Wakristo; la, bwana; mwanamume, aliye mdhaifu sana, ambaye atasimamia madhehebu, na kushikilia pindo za makoti yao, ya Kaisari fulani au Herode, badala ya kushikilia Neno la Mungu. Lakini Mungu anao watu waaminifu, kundi halisi la Mungu, ambao hawajali unavyosema ulimwengu. Huamini kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

74 Hili halipendwi na watu. Hukufanya wewe usipendwe na watu, bali ni Kweli! Ni amri ya Mungu litendeke, na Mungu atalitenda. Mungu awabariki. Sina maana ya kuwakaripia, bali kuwaonya. Ni afadhali kuumizwa kwa moto kuliko kuunguzwa,

wakati wo wote, kwa hiyo tahadharini. Roho Mtakatifu anazungumza katika siku hizi za mwisho.

75 Wote walioandikwa katika Kitabu wataliepuka. Sasa tunaona, lile kundi dogo liko tayari kwa Nguvu ya kuliinua hilo juu angani, kuokoka na dhiki yote hii.

76 Mtu fulani alisema, majuzi wakati nilipokuwa ninazungumza, kasema, "Ndugu Branham, huamini basi kanisa litapitia kwenye ile dhiki?"

77 Nikasema, "Ninaamini kanisa litapitia, lakini si Bibi-arusi." Kanisa litapitia katika ile dhiki, ndiyo, bwana, lakini Bibi-arusi yu huru nayo. Huyo atanyakuliwa, dakika moja, kufumba na kufumbua. Atanyakuliwa kumlaki Bwana hewani, kwa ajili ya Karamu ya Arusi. Hana kitu cha kumfanya apitie katika dhiki yo yote; Bwana wake amelipia gharama yake. Tunashukuru sana kwa jambo hilo. Ndiyo, bwana.

78 Baada ya kukataliwa, na wote wawili kanisa na taifa, kulikwa na kilio kimoja kilichotokea, kilichofuatia, kilikuwa, "Ondosheni Hilo!"

79 Hicho ndicho kilio cha pili tulicho nacho. Kanisa limemkataa katakata Roho Mtakatifu. Tunajua limemkataa. Lo, washiriki wametoka kwa kila kitu, huo ndio mwito mkuu, wa Kipresbiteri, Kimethodisti, Kibatisti, Kiluteri; bali kanisa, lenyewe, madhehebu, haliwezi kusogea. La, bwana. Tayari limeishaunda madhehebu. Likoje sasa? "Lisulibishe! Lisulubishe!" Nini? Kusulubisha, upya, (nini?) Neno lililothibitishwa, kuwa Ukweli. Neno la Mungu, limesulubiwa, upya. Kama vile tu Hawa alivyochafua ulimwengu wote wa maumbile ya asili, kwa kukataa kijisehemu kimoja kidogo cha Neno la Mungu, vivyo hivyo kanisa limetenda jambo lile lile.

80 Unaweza uniambie, "Ndugu Branham, una tafsiri isiyo sahihi ya jambo Hilo." Vema, hayo ni maoni yako.

81 Mungu hahitaji mfasiri ye yote. Mungu Hujifasiria Mwenyewe. Hiyo ndiyo shida yenyewe, leo, tunao wafasiri wengi mno waliotengenezwa na binadamu. Mungu anaweza kufasiri, Mwenyewe. Thibitisho Lake Mwenyewe la Neno Lake ndilo tafsiri.

82 Pengine Mafarisayo wangepiga kelele, pia, "Tunayo tafsiri!" Msadukayo anasema, "Tunayo!" Lakini Yesu ndiye aliyekuwa ile tafsiri. Amina.

83 Udhihirisho wa nguvu ya Mungu iliyofunuliwa, iliyoahidiwa, ndiyo uthibitisho. Someni Maandiko muone ambalo kanisa linapaswa kuwa leo hii. Ndiyo, bwana. Mungu hahitaji mfasiri ye yote.

84 Hebu na tuzungumze ambalo walimtendea Yesu. Waliona, nyuma huko, kwamba walifikiri Yeye hakuwa na tafsiri. Yeye alikuwa ndiye ile tafsiri. Haikumlazimu Mungu kufasiri

Hilo. Maisha ya Yesu yalifasiri. Yeye alisema, “Yachunguzeni Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani yake; Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Na iwapo sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Iwapo kazi zile zilizonenwa kuhusu siku hii, hazijidhihirishi zenyewe ndani Yangu,” Yeye alisema, “basi msiamini jambo hilo.”

85 Walitenda hilo? Mungu alisema, “Bikira atachukua mimba,” naye alichukua. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika; lakini hawakuamini. “Bikira atachukua mimba,” na akachukua. Ilinenwa, “Viwete watatembea, vipofu wataona,” na jambo ambalo lingetukia. Ilithibitisha wangelilitenda, na Yesu ndiye aliyekuwa lile dhihirisho.

86 Musa akasema, “Bwana Mungu wako, atakuondokeshea Nabii, kama nilivyo Mimi.” Neno humjia nabii. Na, nabii, Neno huyatambua mawazo ya moyo. Walipomuona Yeye akitenda upambanuzi ule, walisema, “Huyu ni Beelzebuli, mpiga ramli.” Hilo si zaidi ya jina walilompa Yeye, jambo lile lile leo, anaitwa “mtakatifu anayejivingirisha,” au kitu kama hicho. Hilo ni kweli.

87 Hata hivyo, Yeye hahitaji tafsiri yo yote. Yeye alikuwa ndiye tafsiri. Mungu alilithibitisha Mwenyewe. Ni mtu gani huyo mwenye dhambi leo, au ni nani huyo aliyekuwa mwenye dhambi wakati huo, ambaye angekana kwamba Neno halikufasiriwa?

88 Yesu aliwauliza, kasema, “Yachunguzeni Maandiko. Yanashuhudia Mimi ni nani. Ndiyo tafsiri. Kama maisha Yangu hayafasiri ninachokizungumzia, basi msiniamini.”

89 Ni mtu gani mwenye dhambi angekuwepo leo, ambaye angeweza kutazama katika Biblia na kuona kama Roho Mtakatifu siye mfasiri wa Neno leo, akijijulisha Mwenyewe kwa udhihirisho wa ahadi za vipawa, na mambo yale ambayo Yeye aliahidi kutenda katika zamani hizi? Malaki 4 ikitimizwa, Maandiko yale mengine yote yakitimilizwa, na kuliona hilo papa hapa katika mwisho wa wakati! Huhitaji mtu ye yote kulifasiri. La, bwana. Hujifasiri Lenyewe. Inathibitisha ndio Ujumbe wa wakati huu! Tubuni mkamrudie Mungu, ulimwengu wote! Ninyi makanisa, tubuni mkamrudie Mungu! Msijaribu kunawa mkamwondoe Yeye kutoka kwenye mikono yenu, sababu hamwezi kulitenda. Jambo lenyewe linaendelea sasa hivi, kama ilivyokuwa wakati huo.

90 Yeye alisema, “Yachunguzeni Maandiko; Yananishuhudia Mimi.” Yesu alisema, “Kazi zangu ndizo mtafsiri Wangu.”

91 Yeye alimwambia Musa, wakati Yeye alipokutana naye juu kule kwenye kijiti kilichowaka moto. Yeye alisema, “MIMI NIKO. Ninakumbuka ahadi Yangu. Ninakumbuka kwamba ningewatoa hao watu, kwa mkono wenye nguvu, nilitoa ahadi,

na ninakwenda pamoja nawe. Ninakutuma. Wewe uwe tu kinywa Changu, na ishara zitafasiri iwapo nilikutuma au la." Amina.

92 Hilo ndilo jambo ambalo linawapasa wanaume na wanawake kutafuta leo, ahadi ya kutoka kwingine, na tafsiri ya Neno la Mungu likidhihirishwa.

93 Shida ya hilo, leo, wao wanasema, "Vema, kanisa langu haliamini Hili." Kuna nini? Unaishi kwenye kivuli cha wakati mwingine. Hayo makanisa yalikuwa mazuri katika nyakati zao, lakini wakati huu je? Huu ni wakati mwingine.

94 Usingemfanya kamwe Wesley amwamini Luther, hapakuwa na utakaso. La, bwana.

95 Usingemfanya kamwe Mpentekoste amwamini Mbatisti, au namna hiyo, kurudia jambo hilo. Walipata kitu bora zaidi. Waliishia nuru yao ya siku yao.

96 Na, leo, Pentekoste imejiundia madhehebu na kuketi chini moja kwa moja kama wao walivyofanya, ni jambo lile lile kabisa. Na Neno linaendelea, na Hilo linaondoka moja kwa moja kutoka kwao. Hilo ni kweli kabisa, sababu tunakuwa wagumu sana na walio kakamaa sana. Tunaachilia makanisa yetu yawe katika hali ya aina yo yote, yanaendelea. "Maadamu tunao washiriki, ni hilo tu lililo la lazima, sababu tuna zaidi ya tuliowahi kuwa nao." Tunajigamba kwa jambo hilo.

97 Hebu niwaambieni jambo fulani ambalo ni mithali ya zamani, kwamba, "Shetani hulihesabu kundi lake, bali Mungu hupima Lake."

98 Hilo ni kweli, pia, hata leo. Mungu anakupima wewe kwa Neno Lake, kuona kama umepungukiwa au la. Siyajali makundi, ni wangapi, jinsi Hilo lisivyopendwa na watu. Ni Neno la Mungu likidhihirishwa kwa saa hii. Sawa kabisa. Sijali kuhusu umati wa watu, na eti ni nani ajaye na nani asiyekuja. Neno la Mungu ndilo lililo hatarini, kama lilivyokuwa pale mahakama ya Pilato. Lipimeni, tuone tumepata nini, mahali ambapo tumepungukiwa. Ndiyo, bwana. Tunaamini kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

99 Tunaona kwamba Yeye alimwambia Musa kwamba, "Nitakuwa pamoja nawe, na nitatumia tu kinywa chako. Wewe nenda ukanene maneno nikuambiyo, na ishara zitajifasiri zenyewe."

100 Unaona, Mungu hahitaji mfasiri ye yote. Loo, la, haimpasi kuwa mfasiri. Tafsiri ya Mungu hujithibitisha Yenyewe. Yeye alisema kwamba Yeye Ndiye mfasiri wa Neno Lake Mwenyewe, na ndivyo alivyo. Yeye alilitenda, kwa Musa, na Yeye hulitenda leo. Tunamjua Yeye, katika Biblia, kama Elohim. *Elohim* ni "Yeye ajitoshelezaye kwa yote." Yeye hahitaji shauri la mtu ye yote. Husimama peke yake. Yeye ni Mungu, na Yeye ni Neno.

Na wakati Neno linapoahidi kitu, na kukithibitisha mbele yako, unataka tafsiri ya namna gani nje ya hiyo?

101 Loo, mwanamume mwenye dhambi au mwanamke, u nani wewe ambaye ungeweza kusimama na kusema kwamba Hilo ni kosa? Ambapo Mungu, pamoja na Roho Wake Mtakatifu na Neno lililoahidiwa, hulifasiri Hili mbele za kila mmoja wetu, sisi tu nani sisi kusema kwamba ni kosa? Salala, ewe mtu mwenye dhambi, wawezaje kufanya hivyo? "'Mwenye dhambi,' unamaanisha nini kwa neno hilo, Ndugu Branham?" Kutokuamini! Kuna dhambi moja tu, hiyo ni kutokuamini. Hahitaji tafsiri ya upuzi ya mwanadamu!

102 Yeye hufasiri Lake Mwenyewe. "Mimi ni Bwana," Yeye alisema, "Nalipanda Hilo; nitalitilia maji Hilo, mchana na usiku, asije mtu akalitoa mkononi Mwangu." Yeye pia alisema, katika Andiko jingine, kwamba, "Yeye aliliangalia Neno Lake, ili alitimize." *Kulitimiza,* "kulifunua" kwa (nani?) Wateule Wake, kwa wale ambao wamepelekwa wapate kuona, ambao wamepelekwa kuliona, hasa. Hulidhihirisha kwa wale ambao wamepelekwa wapate kuona, kuona Hilo.

103 Yeye huliangalia Hilo, hulichunga na tafsiri hizi zote za kipumbavu za kimwili, mambo haya, ambayo, *"Hii* ni sawa, na *ile* ni sawa, *ile* ni sawa." Mungu ni sahihi. Mtu wa Mungu aliyetambulishwa!

104 Wote hao Mafarisayo wangeweza kusimama, waseme, "Sisi ni wa Mungu! Tunazo zile amri. Tuna *hili."* Na hapo lilisimama Neno, Lenyewe. Kasema, "Liondosheni Hilo! Lisulubisheni! Halijitambulishi Lenyewe kwa yale tunayoamini."

105 Lakini lilijitambulisha Lenyewe kwa Neno. Amina. Wale waliokuwa na macho kuona, waliliona. Wale waliokuwa vipofi hawakuliona Hilo.

106 Wala hawataliona leo. Basi. Wanakwenda, wamejifungia nje wenyewe, wengi wao, mbali na Hilo.

Loo, ndiyo, kwa kulitimiliza Hilo, kuonyesha kwamba Hilo ni kweli!

107 Watu wengine husema, "Ninaamini kiasi *fulani* cha Hilo. Ndugu Branham, ninaweza kuamini Biblia. Ninaihurumia Biblia. Mimi huihurumia Biblia. Ninaamini hivi na vile. Ninamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Bali siwezi kamwe kuiamini yote, kwa maana madhehebu yangu husema sivyo ilivyo."

108 Basi una mfasiri wa namna gani? Ni kama yule aliyekuwa naye Hawa, shetani. Yeye alijaribu kumfasiria Hawa Neno, naye akasema, "Loo, *hii* ni kweli, na *ile* ni sawa, lakini hakika . . ." Hakika, ni sawa! Anenalo Mungu, Hilo ni sawa! Mimi sijali jinsi gani Hilo linaonekana kwa wengine. Mungu aliposema litatukia, litakuwa jinsi hiyo. Je, wewe ungemtumia mfasiri wa Hawa? Loo,

ewe mwenye dhambi, ungewezaje kufanya hivyo? Ndiyo, bwana. Wao wana mfasiri wa Hawa.

109 Thibitisho, kama nilivyosema hivi majuzi, tunajaribu kutoa uthibitisho. Luther alisema, "Amini, kisha utoke." Shetani huamini, pia. Wesley alisema, "Paaza sauti, na umempata Huyo," lakini alikuta kwamba hakumpata. Pentekoste ikasema, "Nena kwa lugha, na umempata Huyo." Hawakumpata. Christian Science wakasema, "Ukipendana, una tunda la Roho," lakini hawana. Wao hukana Uungu wa Yesu Kristo.

110 Uthibitisho wa Hilo ni nini? Wakati roho aliye ndani yako anaweza kuitikia kila ahadi kwa amina, na Mungu atalitimiza. Hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa na Yesu Kristo. Naam, ndiyo. Walikuwa, walikuwa na matunda zaidi ya roho, walikuwa na thibitisho za kila aina. Huwezi kushikilia uthibitisho wo wote kwa kitu cho chote ila Mungu Mwenyewe akidhihirisha Neno Lake. Huo ndio ushahidi pakee wa kweli uliopo kwamba wewe u Mkristo. Wawezaje kuwa Mkristo wakati . . .

111 "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu. Yeye yule jana, leo, na hata milele!" Yeye ndiye Mungu yule yule aliyekuwa ndani ya Daudi. Yeye Ndiye yule yule aliyekuwa katika Musa. Yeye ndiye Mtu yule yule aliyekuwa katika mitume wote. Na Yeye ndiye Mtu yule yule aliyekuwa katika Yesu Kristo, kujidhihirisha Mwenyewe pale kwa Neno lile lililoahidiwa. Na Yeye ni Mungu yule yule leo, Neno lile lile, likitoa Nuru juu ya Neno la wakati huu. Mungu aturehemu! Ndiyo, bwana. Kumwamini Mungu kujifasiri Mwenyewe, kila Neno kuthihirishwa! Ndiyo, Yeye ndiye anayejifasiria Mwenyewe.

112 Na, ndugu, ninaiwazia saa hii! Ningeweza kukaa kwenye hili muda mrefu, lakini mna mkutano unaokuja. Ninaamini, na nitasema, leo; iwapo hatuangalii, Yeye yuko mikononi mwetu sisi Wamarekani. Lifikirie hilo. Sisemi hili kwa hasira; nanena hili kwa ajili ya Nuru. Ninasema kwamba Damu ya Yesu Kristo iko juu ya kanisa la Amerika leo. Damu ya Yesu Kristo iko juu ya Amerika, yote. Damu ya Yesu Kristo inapinga Mmethodisti, Mpresbiteri, Mluteri, Wapentekoste. Iko katika mikono yetu sisi sote. Hebu na tuone kama ndivyo ilivyo sasa. Fikiria hilo, Damu ya Yesu Kristo! Lo, jamani!

113 Na kama vile Pilato siku ile, inanikumbusha njia tatu ambazo Pilato alijaribu kuiondoa Hiyo mkononi mwake. Alijaribu njia zote tatu kuiondoa Hiyo mikononi mwake lakini alishindwa. Kuna njia moja tu ya kuiondoa kwenye mikono yako. Hebu tuone alilotenda. Pilato alijaribu hizi njia tatu, na zote zilishindwa.

114 Lazima tukabiliane na kisa hiki. Twajua ipo hapa, kwani Neno Lake limekwisha tambulishwa kwa ushuhuda wa

Maandiko. Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii limefanyika mwili, hata ile sehemu ya uovu ya kumkataa Yesu Kristo; na Yeye, katika Wakati huu wa Laodikia, yuko nje ya kanisa. Tunajua huo ni Ukweli. Fikiria hilo, Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, mikononi mwetu. Wewe . . . Hilo linanitisha, kuliwazia. Kumchoma Yeye, inaleta simanzi, kuwazia, Damu ya Yesu Kristo!

115 Wakati, mtu ataangalia damu ya binadamu mwenzake. Wakati mmoja huko Chicago, si muda mrefu uliopita, rafiki yangu fulani alikuwa amesimama pale wakati mmoja wa—wa shirika la Dillinger, au cho chote kile, alipigwa risasi barabarani. Watu walikuwa wamekusanyika, kwa mamia, nao walisimama pande zote. Lakini, wao, walifanya nini? Mahali damu ile ilipoenea barabarani, kwa tundu lile la risasi, kila mtu alitembea kando ya damu ile. Wasingeikanyaga damu ya binadamu mwenzao. Ah, la, bwana. Wanashuku sana jambo hilo.

116 Bali watakanyaga moja kwa moja Damu ya Yesu Kristo. Usemi huu wa zamani bado ni wa kweli, "Wapumbavu watatembea kwa viatu vyenye misumari mahali ambapo Malaika wanaogopa kukanyaga." Hilo ni kweli, watatembea moja kwa moja juu Yake, wakisema "Siku za miujiza zimepita. Hilo lilikuwa sawa kwa mitume, lakini si kwa ajili yetu." Loo, jamani, wawezaje kusema hilo? Unakanyaga chini ya mguu Damu ya Yesu Kristo ambayo ilikutakasa! Loo, jamani, fikirieni kuhusu Damu mikononi mwetu!

117 Wakati, damu ya mwenzako. Ninafikiria kuhusu siku nyingi zilizopita, majuma machache yaliyopita, tulipofikiria lisingeweza kutukia katika taifa letu. Vipi kumhusu jamaa huyu, Oswald? Akikaa mle katika rumande, huku wanawaza na kuwazua, kama yeye ana akili timamu.

118 Na ninamfikiria mtu ambaye angesikiliza kanda hii, au anayeketi hapa, mahali po pote, na kusikiliza Ujumbe huu, akiuhakikisha, akiwaza na kuwazua, akijua kwamba yakubidi upitie hukumuni na uwajibike kwa Neno la Mungu, uwajibike kwa Damu ya Yesu Kristo, ambayo umejulishwa, ikiwa mikononi mwako, mikononi mwetu.

119 Mwangalie Oswald ameketi pale, lingepaswa kuwa jambo la kutisha jinsi gani kwake, au lingelikuwa hivyo, au nadhani lilikuwa, alipofikiria kwamba angeyakabili Mahakama Kuu iliyo na hasira ya kumuua Rais wao. Kusingekuwa na rehema. Ushuhuda wo wote wangeweza kuupata dhidi yake, ungeshindiliwa dhidi yake. Alama za vidole, bunduki, mahali alipokuwa, yote yangeletwa mbele zake.

120 Hilo ni jambo jepesi sana ukilinganisha na itakavyokuwa kwa watu ambao wameketi katika mikutano hii na kumwangalia Yesu Kristo akiinuka kwa umbo la Utu Wake, na kujitambulisha Mwenyewe, nawe unatoka bila ya kumkubali Yeye, ukishikilia

kanuni ndogo ya imani fulani, au jambo fulani uliitalo dogo. Hilo litakuwa jambo jepesi, uketipo kwenye Uwepo wa Mungu mwenye hasira, wewe ambaye umekanyaga ile. . . Wewe ambaye umekanyaga Damu ya Mwanawe, na kumsulubisha Yeye upya bongoni mwako, kabadilisha haki yako ya mzaliwa wa kwanza na kupendwa na watu. Litakuwa jambo la kutisha siku ile. Litakuwa ni wazo la kutisha. Unawezaje kuketi katika rumande ya kutokwa na jasho?

121 Enyi wenyeji wa Afrika, ninyi mlioko Australia, Sweden, Uswisi, ninyi ambao mtasikiliza kanda hii, mtajibuje kwenye Siku ya Hukumu, na huku nimekuwepo nchini mwenu na mmeona utambulisho wa Yesu Kristo akisimama miongoni mwa watu, akijithibitisha Mwenyewe?

122 Jasho, jamani, lazima ametokwa na jasho! Jamani, angewezaje kufanya hivyo kama alikuwa na akili timamu?

123 Unafikiri itakuwa Mungu mwenye hasira jinsi gani kwa wale ambao wamemkanyaga chini ya miguu yao Mwana wa Mungu, na kumsulubisha Yeye upya, tena?

124 Angalia, rubani, anapokuwa tayari kurusha ndege juu. Rubani ataitoa ndege nje, atachunguza kila kitu kabla ya kuondoka, kila chombo. Atatoka aende kwenye njia ya kurukia, na kusimama nje huko na kuchunguza vijimbawa vya kurukia, anachunguza vifuniko vya mafuta. Kila kitu, kila chombo alicho nacho, anakichunguza tena na tena. Wengi wenu mmesafiri kwa ndege, nanyi mnajua hilo ni kweli. Yeye hukichunguza kila chombo. Kwa nini? Ana damu ya binadamu wenzake mikononi mwake. Anataka kujua yakini kwamba kila kitu kinachowezekana kinafanya kazi barabara.

125 Je, vipi daktari katika upasuaji, ajuapo kwamba yeye anakwenda kumpasua mtu, kuondoa uvimbe au moyo, au kitu kingine, na kufanya upasuaji? Anapokwenda kupasua mwili wako, atachunguza moyo wako, atachunguza msukumo wako wa damu, atachunguza iwapo ina homa yo yote, atachunguza nusukaputi. Atachunguza kila kitu, tena na tena, na kurudia tena. Kwa nini? Hataki damu ya binadamu mwenzake mikononi mwake.

126 Na iwapo daktari na rubani, na kadhalika, watachunguza, Kanisa la Yesu Kristo linapaswa kutendaje, tuonapo mambo ambayo tunamoishi leo? Afadhali tuchunguze. Damu ya Yesu Kristo yaweza ikabakia mikononi mwetu.

127 Sasa hebu tuchukue jambo moja, hila ya kwanza ya Pilato, ilikuwa, "Sioni kosa ndani Yake."

128 Jinsi hilo lilivyo miongoni mwa mengi ya makundi mazuri leo! "Sioni kosa katika Neno. Liko sawa, ila hilo lilikuwa kwa ajili ya mitume." Biblia ilisema Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Unasema, "Biblia hiyo ni sahihi. Ninaamini walinena kwa lugha; ninaamini wao waliwatoa pepo; ninaamini

walitambua mawazo; naamini kulikuwa na manabii; lakini sio siku hizi." Ee, bwana, ewe mwenye dhambi, una nini? Kunatendeka nini wakati Mathayo ya 28, 24:24 iko wazi moja kwa moja? Waebrania 13:8 inaporuka tena moja kwa moja pajani mwako.

129 Pilato, hakuweza kuinawa Hiyo kuiondoa mikononi mwake namna hiyo. La, bwana, ilimrudia moja kwa moja pajani mwake tena. Hivyo ndivyo itakavyomrudia kila mtu, wakati uliposimama na kumwona Mungu akitimiza ahadi Yake.

130 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, na mbatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

131 Umbali gani? "Ulimwenguni kote, kwa kila taifa." Kasema Hilo lilikuwa kwa kila taifa. "Enendeni ulimwenguni kote." Halijafikia huko bado. "Hubirini Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

132 Utalinawaje Hilo uliondoe mikononi mwako? Huwezi kutenda hilo. Hilo limethibitishwa, na kutupwa moja kwa moja pajani mwako. Hilo hukurudia, kama lilivyofanya kwa Pilato. Loo, ndiyo, bwana, linakurudia tena, unapoona Maandiko yamethibitishwa moja kwa moja mbele yako.

133 Pili, huku tukimalizia. Pili, tunaona kwamba, kulikuwa na njia nyingine Pilato aliyojaribu kufanya, hivyo ndivyo wafanyavyo watu leo, akalirusha kwa akina Herode wake na akina Kaisari wake. Wahudumu wengi wazuri leo, Mpiskolipani, Mpresbiteri. Mluteri, Mbatisti, Wapentekoste, na kadhalika, wanalirusha kwa mtu mwingine, "Makao yangu makuu ndiyo ambayo hayataniruhusu mimi nitende jambo hilo." Lilimrudia. Linarudi tena leo.

134 Siwaulizi Assemblies of God, Umoja, Church of God, Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri. Ninakuuliza wewe, kama mtu binafsi, unatenda nini na Damu ya Yesu Kristo? Tutafanya nini na Neno hili la Mungu lililopakwa mafuta ambalo lipo papa hapa mbele yetu leo, ambalo twajua lapaswa kuwa, ni Kristo, ahadi ya wakati huu? Utafanya nini na Hilo? Si jambo ambalo kanisa lako linatenda na Hilo. Kaisari wako na Herode wako hawahusiani nalo. Hilo halikumpatia Pilato msamaha. La, bwana. La, bwana.

135 Hao Mafarisayo tangu siku hiyo walisema, "Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu." Ndivyo ilivyo. Hilo ni kweli kabisa.

136 Yeye, Yesu, aliwaambiaje? "Mwaweza kuutambua uso wa mbingu, lakini, ishara za zamani hizi hamwezi kuzitambua."

137 Na, loo, sisemi hili kwa Phoenix, bali ninalinena kwa ajili ya po pote linapotaka kwenda. Enyi Mafarisayo vipofu! Mwawezaje, huku mkitumia mamilioni ya dola, mnaweza kuutambua ukomunisti; bali Neno la Mungu, lililothibitishwa kwa saa hii, hamwezi kulitambua? Mnalisulubisha Hilo tena. Mnajua yote kuhusu ukomunisti; kama mngelijua Biblia yenu, mngejua jambo hilo lingebidi kutukia. Hilo mimi halinivutii. Ninachukia ukomunisti. Nachukia kitu cho chote kipingacho Mungu. Lakini shauku yangu ni hii, Kanisa liwe tayari kwa ajili ya saa hii, kwa ajili ya kuondoka kwa Bibi-arusi.

138 "Kuutambua uso wa mbingu, bali ishara za wakati huu hamwezi kuzitambua."

139 Na kwenye hukumu Yake leo, ipo kwenye mahakama ya Taifa kuiunda hii Halmashauri ya Makanisa, na kila kitu. Mwaweza kuutambua ukomunisti na mambo yote haya ambayo wahubiri wanahubiri juu yake; na kutembea juu ya ishara za wakati huu, na kuliita Hilo "wenda wazimu," mnaliita Hilo "uwezo wa kushirikiana mawazo," au kitu kama hicho, na kuondoka, na kuwazuia watu wao kuja na hata kulisikiliza Hilo. Kama historia haikujirudia yenyewe, mimi, jina langu si William Branham. Kabisa. Kutatukia nini? Linaitupa Damu ya Yesu Kristo moja kwa moja kwenye mikono yenu, nanyi mnaiita Hiyo "roho mchafu," kama walivyofanya wakati huo.

140 Ulimwenguni pote! Nadhani mnajua ninalomaanisha basi. Kila mahali! Kwa nini mlinikataa, huko Uswisi? Kwa nini mlilitenda, Finland? Damu itakuwa juu ya mikono yenu. Hiyo ni juu yenu. Si mimi, hamkunikataa; mlimkataa Yeye, si mimi, kwa sababu mlisema, "Siamini *hilo*." Neno husema hivyo! Basi. Mafarisayo vipofu, wanaweza kutambua ukomunisti, kutambua mambo yote haya, lakini, saa wanayoishi, hawawezi kuitambua. Hili ni kweli kabisa.

141 Sasa inakaribia kufikia (jamani!) lengo lake la mwisho tena. Saa iliyo muhimu sana imewadia tena. Ni kitu gani? "Msulubisheni! Tutafanya...Hatuwezi kuwafanya wote Wamethodisti; hatuwezi kuwafanya wote Wabatisti; hatuwezi kuwafanya wote wa Umoja; hatuwezi kuwafanya wote wa Utatu; hatuwezi kuwafanya wote *hivi*, *vile* au *lile jingine;* lakini tunaweza kuwa na halmashauri." Ambapo, hampatani kabisa kama vile Mashariki ilivyo mbali na Magharibi, na jambo lote ni kosa. Ni kibaraka wa Rumi. Hilo ni kweli kabisa.

142 Sasa, kama mtu binafsi, nitawaulizeni. Utalitendaje Neno hili lililotiwa mafuta ambalo ni Kristo, Neno lililoahidiwa siku hii? Wewe, kama mtu binafsi?

143 Pilato kamwe hakuliondoa mikononi mwake. Unajua hilo. Alipiga kiyowe, akapaza sauti, na kila hila angeliweza kufanya. Alishindwa kufanya hivyo. Kuna hadithi huko Uswisi, ambapo kiji...maji ya samawati hububujika juu, hapo alipojiua.

Mwajua historia yake. Hatimaye alirukwa na akili, kisha akajiva. Kwa nini hakutubu? Hangeweza kutubu, kama vile Esau asingeweza kutubu. Tayari amelitenda hilo! Usiliache hilo likupate.

144 yeye yuko mikononi mwako. Kazi imetendeka, Biblia inahubiriwa, Roho Mtakatifu amethibitisha Hilo. Mtu ye yote mwenye dhambi, usingethubutu kusema sivyo ilivyo, Roho Mtakatifu katika siku hizi za mwisho! Na Maneno ambayo yamenenwa, akasema yangetimia, basi Hili papa hapa mbele yetu.

145 Usijaribu kulitenda. Usiache mwisho wako uwe kama wa Pilato. La. Laiti angelimpokea Yeye moyoni mwake. Hiyo ndiyo njia pekee unayoweza kumwondoa Yeye mikononi mwako, ni kumchukua Yeye moyoni mwako. Loo, usifanye kosa lile lile.

146 Sikiliza, Waebrania 10 inasema hivi, "Kama tukitenda dhambi makusudi, kutokuamini makusudi, baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Kama ukifanya dhambi makusudi baada ya Hilo kuthibitishwa kwako, halafu unalikataa Hilo, huna nafasi kabisa ya kutubu tena.

147 Hebu kidogo, nina maandishi machache hapa ninayotaka kuyaleta mbele zako kabla sijamalizia.

148 Kama wale wapelelezi waliokuwa wakisafiri kuelekea nchi ya ahadi. Walikuwa katika kutoka, wakitoka Misri, wakitoka kwa Neno la ahadi la Mungu. Mungu alimjulisha nabii Neno Lake, Musa, akampeleka chini kule. Yeye alithibitishwa kwamba Yeye alikuwa ndiye Mungu atakayemtoa kwenye hali zile ambazo aliahidi, yule "MIMI NIKO."

149 Walipofikia nchi ya mpakani, Kadesh-barnea, kosa kubwa walilotenda, walipofika kwenye nchi ile na kuangalia katika nchi ya ahadi, wakasema, "Hatuwezi kuiteka." Wale kumi wengine walikuwa nini? Waliangalia hali ya mambo, sifa ambayo wangelipoteza. "Sisi ni panzi, mbele yao."

150 Lakini Yoshua na Kalebu wakachunguza. Walirudi kwenye Neno, na Bwana alisema, "Ninawapa nchi hii! Ni nchi nzuri, imejaa maziwa na asali." Hawakujali ilionekanaje, *hii* ilikuwa nini, na uhakika *huu* ulikuwa nini. Neno la Mungu lilisema, "Ninawapeni hiyo! Nendeni mkaitwae!" Nao ndio pekee walioingia.

151 Jamani, hebu na tuchunguze ahadi za Mungu za siku ya leo. Hilo ni kweli. Kumbukeni, tuko katika kutoka kwingine, wakati; kutoka, wakati huu, si kuingia nchi ya ahadi ya duniani, bali katika Nchi ya ahadi ya Utukufuni, ambapo hakuna kurudi tena. Atukuzwe Mungu, tutakuwako huko! [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Utafanya hivyo, tunapoviinamisha vichwa vyetu?

152 Nitauliza swali hili wakati kila mwanamume na mwanamke amekaa kimya. Utamtendaje huyu Yesu aitwaye Kristo? Utamkubali Yeye? Utamkubali Yeye kama Mwokozi wako? Je, utakuwa . . . Au, utanawa umwondoshe Yeye mikononi mwako? Je, utajaribu kulipisha, "Vema, kanuni ya imani ya—yangu haisemi Hili," au, "madhehebu yangu hayaamini Hilo namna hiyo"? Iko mikononi mwako kabisa. Huwezi kulikwepa Hilo. Utamtendaje Yesu aitwaye Kristo? Damu Yake iko mikononi mwako, tangu juma hili mkutanoni.

Hebu tuombe.

153 Bwana Yesu, tusaidie sasa hivi katika saa hii. Jalia neema Yako na rehema ikae pamoja nasi. Jalia kusanyiko hili lione, Bwana, kwamba Wewe ni Mungu, na hakuna mwingine ila Wewe. Jalia Nguvu za Mungu sasa, Neno, lijitambulishe Lenyewe, katika watu hawa, ili kwamba ijulikane kwamba Wewe u Mungu, na kwamba nimesema Kweli, Bwana. Nimelitenda, hili, kwa amri Yako; kama Eliya alivyosema zamani za kale, "Nimetenda yote haya kwa amri Yako." Tujalie, Bwana, kwamba iwe hivyo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kila mmoja wenu.

154 Roho Mtakatifu ndio tu amenikatiza, dakika chache zilizopita, nilipoanza kuomba. Yeye alisema, "Kuna baadhi ya watu hapa ambao hawajui jambo hilo bado." Mungu wa Mbinguni na awaacheni bila cho chote, na alitupie Hilo moja kwa moja pajani mwenu leo, basi.

155 Ninyi watu mlio wagonjwa hapa. Sijawahi kutenda hili kwenye mkutano wa Wafanyi Biashara. Ninyi watu wagonjwa hapa, mnaomwamini Mungu, na mnaamini mna imani ya kugusa vazi Lake. Na, kumbukeni, Biblia ilisema, katika Waebrania 4, "Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, huyatambua mawazo yalioko moyoni." Sote twajua hilo. Mnaamini Hivyo? Mtaomba?

156 Hebu mtu ye yote asisogee tangu sasa na kuendelea. Hebu kila mmoja awe na kicho sana, iweni kimya kabisa, kimya kabisa. Ombeni. Roho Mtakatifu sasa na atuelekeze katika jambo la kufanya na la kusema, kwa maana saa hii muhimu sana imewadia hapa sasa dhidi yetu.

157 Bwana Yesu, liko mikononi Mwako. Niko mikononi Mwako. Najitoa mwenyewe Kwako. Litupe Hilo ukalirudishe pajani mwao Bwana, Lirudishe Hilo. Hakika, Roho Wako Mtakatifu mkuu ananiambia hapa kilicho sahihi na kisicho sahihi. Na najua kanda hii itakutana na wengi nje huko, basi naomba kwamba Wewe utajalia ijulikane leo kwamba nimewaambia Ukweli, nami nimetumwa kwa ajili ya jambo hili, kama Wewe ulivyosema mtoni wakati ule wakati Malaika wa Bwana aliposimama pale katika ile Nguzo ya Moto. Na ijulikane leo kwamba nimesema Ukweli, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

158 Inueni vichwa vyenu sasa. Tazameni huku, na msitie shaka. Mungu Mwenyezi na awe hakimu wetu.

159 Yesu Kristo aliposimama hapa duniani! Wakati Yeye alipokufa, Yeye aliponya wagonjwa, Yeye aliokoa waliopotea. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Lakini Yeye alipokuwepo hapa, jinsi walivyojua Yeye Ndiye, ni kwa sababu Yeye alikuwa Neno. Wangapi wanajua hilo ni kweli? ["Amina."] Yeye alikuwa Neno, na Neno huyatambua mawazao yaliyomo moyoni. Hilo ni kweli? ["Amina."]

160 Siwezi kuona mtu katika jengo hili, wakati huu, nimjuaye, isipokuwa wachungaji hawa, na kadhalika, nyuma hapa.

161 Au, labda Ndugu Roberts yupo hapa, nitamtaka tu aanzishe mstari wa maombi. Ndugu Roberts amerudi hapo? [Mtu fulani anasema, "La."—Mh.] Hayupo hapa. Sawa.

162 Huduma yangu itafaa kwa wakati huu. Ninawahimiza, katika Jina la Yesu Kristo, kuniamini mimi, kwamba nimenena Ukweli kuhusu Neno, na muamini kwamba niliyosema ni Ukweli. Mtafanya hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Lijalie hilo, Bwana, lijalie hilo.

163 Kuna mtu aketiye papa hapa. Nawatakeni myageuze macho yenu, hamwezi kuiona Nuru ile inayoning'inia pale? Kuna mtu aketiye pale, anayeniangalia, akiomba. Anaugua ugonjwa wa pafu, na unyonge. Usilikose, bwana. Bw. Carr, inuka na ukubali uponyo wako. Yesu Kristo anakuponya. Sijamuona huyo mtu, maishani mwangu.

164 Kuna mtu nyuma kule, mzuri sana, alikuwa anaomba pia. Lakini mtu yule ana kitu gani, mtu yule pale ana shida ya jicho. Ana uvimbe upande wake wa kushoto. Jina lake ni Bw. Bartlett. Unaamini! Hilo ni kweli, bwana? Mimi ni mgeni kwako? Punga mkono wako; sote tu wageni. Hilo ni kweli. Mungu akubariki. Amini, utapona.

Mnaamini! [Ndugu Branham anatulia kidogo—Mh.]

165 Ulimwambia hilo kwa nini? Unaniamini mimi kuwa nabii Wake, bwana? Ndiyo, bwana. Unaumwa na wasiwasi wa kiroho, umepata wasiwasi kidogo katika biashara na mambo mbalimbali. Hilo ni kweli. Hilo ni kweli. Bw. Carlson, unaamini kwa moyo wako wote kwamba Yesu atakunyoshea jambo hilo? Hilo ndilo jina lako? Hapo ni mahali pako? Sawa, unaweza kupata ulichoomba. Amina.

166 Mtu fulani juu *hapa* aliamini Hilo, amina, mtu fulani aliye na imani halisi ya Roho Mtakatifu.

167 Bibi Waldroff, ninaona hilo. Mimi, ninakujua. La, si kwa ajili yako. Ni kwa ajili ya mtoto yule, na mtoto yule ni mjukuu wako. Sijawahi kumwona, katika maisha yangu. Huo ni ukweli. Mtoto huyo ana ugonjwa wa jicho uliosababishwa na mwasho aliokuwa nao. Hilo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini!

168 Bibi, u mgonjwa sana. Una wasiwasi, una shida ya tumbo, karibu ushikwe na ugonjwa wa neva. Unaamini kwamba Mungu atakuponya? Mary, amini kwa moyo wako wote, na Yesu Kristo atakupa shauku yako.

Yeye yuko pajani mwako!

169 Hapa yupo bibi mdogo anayeketi hapa, anaomba, akinitazama moja kwa moja, kichwa kimeinamishwa. Inuka unitazame. Mtu mzuri. Hukai humu. Unatoka mahali mbali na hapa, New York. Lakini kama utaamini kwamba Yesu Kristo anakufanya mzima, Yeye atakupa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unaamini hilo? Bibi Bryan kutoka New York, amini kwa moyo wako wote, na unaweza kumpokea Roho Mtakatifu sasa hivi.

170 Liko mikononi mwenu, marafiki! Mnaamini Hilo. Neno likijidhihirisha Lenyewe? Mnamwamini Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele? Siwajui watu hawa. Mungu ndiye Hakimu wangu, siwajui watu hawa. Yesu Kristo anawajua. Utafanya nini na Neno hili lililotiwa mafuta, kama Yeye alivyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu"? Kama sehemu hii ni kweli, Ujumbe ninaouhubiri ni kweli. Ni Roho Mtakatifu, Mwenyewe, akifanya tafsiri Yake Mwenyewe, kwamba ni sahihi. Amina. Amini Hilo kwa moyo wako wote! Utafanya hivyo?

171 Simama kwa miguu yako basi na ukubali Hilo, katika Jina la Yesu Kristo.

172 Wakati Roho Mtakatifu yupo hapa, nataka kuwekea mikono vitambaa hivi hapa. Hebu tumwinulie Kristo mikono yetu.

173 Bwana Yesu, tunakuamini Wewe. Tunajua Wewe U Kweli, Nuru ile, Neno. Naweka mikono yangu juu ya leso hizi. Naomba, Bwana Yesu, kwamba nguvu Zako zitalizunguka jengo hili naa kupitia juu ya leso hizi, juu ya makoti haya na majoho haya. Roho Mtakatifu na aje juu yao, Bwana. Lijalie. Na jalia waponywe, kila mmoja wao, kwani Neno Lako ni Kweli. Lijalie, Bwana.

174 Sasa kwa kila mmoja katika kusanyiko hili, utamtendaje huyu Yesu aitwaye Kristo? Liko mikononi mwako. Usiache watu wakuambie. . . Ninamaanisha watu wanaosikiliza kanda hii, watu nje ya hapa mkutanoni, utafanya nini nalo leo? Kwa nini usimkubali Yeye, kila mgonjwa ndani hapa? Kila mwanaume mwenye mashaka humu ndani, kila mwanamke mwenye mashaka, kwa nini usimkubali Yeye kama Mwokozi wako? Hutamnawa kamwe umwondoe mikononi mwako. Kanuni ya imani yako haitamwondoa Yeye kamwe. Hakuna sabuni ya kutosha ya Fuller nchini kuiondosha Hiyo. Kitu kimoja tu unaweza kufanya, mwingize Yeye moyoni mwako! Amina. Mtalikubali? Inueni mikono yenu basi, mkaseme, Yeye apewe sifa na utukufu.

175 Baba wa Mbinguni, hao ni Wako. Neno Lako limetambulishwa. Watu hao ni Wako. Nawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

176 Inueni mikono yenu sasa na mpeni Yeye sifa. Nami namkabidhi Yeye kwenu, katika Jina Lake Yesu Kristo.

*Tumtendeje Huyu Yesu Aitwaye Kristo?* SWA64-0126
(What Shall We Do With This Jesus Called Christ?)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, Januari 26, 1964, katika Ramada Inn kule Phoenix, Arizona, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org